^Q=_êçÅÜiêÉ=pt^KéÇÑ===O===TLNTLNT===QWQS=mj



# MRADI WA BOMBA LA MAFUTA GHAFI LA AFRICA MASHARIKI (EACOP)

Mwaka 2006, mafuta ya kutoshereza kibiashara yaligundulika kuwepo katika bonde la Ziwa Albert nchini Uganda. Waendeshaji wa shughuli za mafuta nchini humo: CNOOC LTD, TOTAL na Tullow PLC wamekamilisha awamu ya uvumbuzi na sasa wanaelekea katika uendelezaji, ambao utaelekeza uzalishaji wa rasilimali hiyo ya mafuta nchini Uganda.

Mara baada ya kuzalishwa, sehemu ya mafuta ghafi itasafishwa nchini Uganda na kusambazwa kwenye soko la ndani na kiasi kingine kusafirishwa katika soko la kimataifa. Usafirishaji kwenda soko la kimataifa utatumia njia ya bomba la mafuta ghafi, liitwalo "Bomba la Kusafirishia Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki" (The East Africa Crude Oil Export Pipeline – EACOP). Bomba hili litajengwa na kuendeshwa na Kampuni ya Bomba la Mafuta kwa ubia na Kampuni ya Taifa ya Mafuta ya Uganda (NOC), Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) na Makampuni matatu ya mafuta, CNOOC, TOTAL na TULLOW.

# Mradi wa EACOP

**EACOP ni bomba la kusafirishia mafuta lenye urefu wa kilomita1,445 ambalo litasafirisha mafuta ghafi ya Uganda kutoka Kabaale nchini humo hadi rasi ya Chongoleani iliyo karibu na bandari ya Tanga nchini Tanzania.**

- Njia ya bomba ilichaguliwa naSerikali ya Uganda ikiwa ni ya gharama nafuu na yenye uimara.
- Kutokana na asili ya mafuta ghafi ya Uganda kuwa nta na yenye mnato, bomba litahitaji kuwa na joto kwenye njia nzima, nakufanya bomba la EACOP kuwa refu kuliko yote duniani lenye mfumo wa joto.
- Bomba litafukiwa chini ya ardhin kupunguza athari kwenye mazingira.
- Baadhi ya vituo vitakuwa juu ya ardhi na kuundwa ilikupunguza athari kwa mazingira na jamii.
- Mradi utazingatia sharia za kitaifa za nchini ya Uganda na Tanzania na matakwa ya kimataifa.
- Kituo cha kuhifadhi na kupakia mafuta kwa ajili ya usafirishaji baharini vitawekwa kaskazini mwa Bandari ya Tanga kwenye rasi ya Chongoleani.




**UGANDA** | Urefu wa km **296**, Mikoa **9** na Wilaya **24**

**TANZANIA** | Urefu wa km **1,149**, Mikoa **8** na Wilaya **24**

# Ratiba za mradi wa EACOP




| 1,445km | 1.2m | 216Kbd | 6 | 2 | 53 |
|---|---|---|---|---|---|
| BOMBA LA KUSAFIRISHIA | KUZIKWA CHINI YA ARDHI | KIWANGO CHA KUSAFIRISHA MAPIPA KWA SIKU | VITUO VYA KUSUKUMA | VITUO VYA KUPUNGUZA MSUKUMO | VITUO VYA VALI ZA KUFUNGA |

# Awamu ya Ujenzi

Mara tu Uamuzi wa Mwisho wa Uwekezaji (FID) kufanyika, ujenzi wa bomba utaanza na utadumu kwa miezi 36.

Ujenzi utajumuisha:

## 1. Ujenzi wa Bomba

Ujenzi utafanyika kama inavyoonekana katika mchoro hapa chini. Mara litakapo kamilika, bomba litawekwa kwa umakini katika mfereji uliochimbwa awali au, katika baadhi ya maeneo litahitaji kuchimbiwa kwa mlalo chini ya mkondo wa maji au barabara.




## 2. Ujenzi wa Vituo vya Muda

Vituo vingine vitakavyojengwa ni kama vile;

- Vituo kwa ajili ya kufunikia bomba na eneo la kuhifadhi mabomba
- Ujenzi wa eneo la kazi za ziada (mafuta, eneo la kutuahelikopta, taka)
- Mabwawa ya kufanyia majaribio, barabara, mashimo ya vifaa vya ujenzi

## 3. Ujenzi wa kituo cha kuhifadhi mafuta na gati



Mafuta ghafi, yatakayosafirishwa kwanjia ya bomba yatahifadhiwa katika kituo kitakachowekwa eneo la Chongoleani katika ghuba ya Tanga, kabla ya kusafirishwa na kuuzwa katika nchi nyingine. Vyombo hivyo vya kubeba mafuta ghafi vitakuwa mahali pa usalama kwenye kilindi cha maji.

# UPATIKANAJI WA ARDHI

Ardhi itahitajika ili kujenga bomba la EACOP na vituo husika. Ardhi hii itahitajika ama kwa muda mfupi au muda wa kudumu.

## Upatikanaji wa ardhi kwa matumizi ya muda mfupi

- ndani ya takriban upana wa mita 30za njia miliki kwa ajili ya ujenzi
- kwa vituo vya muda vya juu ya ardhi (kama makambi ya ujenzi).
- Ardhi itakayohitajika kwa muda mfupi itakodishwa kwa takribani miaka 1- 4 nakurejeshwa kwa mmiliki katika hali yake ya awali.

## Upatikanaji wa ardhi kwa matumizi ya kudumu

- Ardhi itakayohitajika kwa matumizi ya kudumu kwa usimikaji vituo juu ya ardhi (vituo vya kusukuma, vituo vya kupunguza msukumo na kituo cha kuhifadhi mafuta) pamoja na njia miliki ya kudumu.
- Baada ya ujenzi, bomba la EACOP litahitaji kuwa na njia yenye umiliki wa ardhi kisheria ikiwemo uthibiti katika ukanda wa usalama.

Mradi wa EACOP unajidhatiti katika:

- Kufuata sheria husika za kitaifa na matakwa ya kimataifa.
- Kuhakikisha wamiliki wa ardhi na watumiaji wote wanaoishi ndani ya njia ya bomba wataheshimiwa na kupewa fidia stahiki.
- Watu walioko katika hali tete wanatambuliwa nakusaidiwa ipasavyo.
- Kufikia makubaliano na kila kaya itakayoathirika, kutoa fidia na programu ya urejeleshaji shughuli za kujikimu na kusaidia kaya kuhama katika maeneo (kwa wale ambao watachagua kurejeshewa makazi kama aina ya fidia kwaajili ya urejeshaji makazi, kuwasaidia kuhama kwenye maeneo mapya).

^Q=_êçÅÜìêÉ=pt^KéÇÑ===P===TLNTLNT===QWQS=mj



DELEZA

AFUTA AFRIKA MASHARIKI

YA MAFUTA AFRIKA MASHARIKI

# Kujidhatiti katika Ulinzi wa Mazingira

Mradi wa EACOP utahakikisha kwamba masuala ya afya, usalama, ulinzi, jamii, uchumi na mazingira yameshughulikiwa katika awamu zote ikiwemo upangaji, ujenzi, na uendeshaji wa bomba.

Njia ya bomba imechaguliwa kuepuka maeneo mengi yenye mazingira nyeti kama hifadhi za taifa na maeneo yenye idadi kubwa ya watu.
Vituo vitawekwa mahali salama na kuendeshwa ili kupunguza uwezekano wa athari kwa sura ya nchi na ikolojia.

Tumetengeneza hati juu ya bayoanuwai ambayo imeanisha kanuni zetu za kazi.

Kwa mujibu wa hati hii, shughuli zote za EACOP zitafanyika kwa:

- KUEPUKA athari zisizo za lazima kwenye mazingira, bayoanuwai, na jamii za wenyeji.
- KUPUNGUZA athari za kuepukika kwenye mazingira, bayoanuwai na jamii za wenyeji.
- KUONDOA athari yoyote baki, ambayo inaweza kuwa bado ipo.

MFUMO WA KUPUNGUZA ATHARI




# Kujidhatiti kuleta Maendeleo Kijamii - Kiuchumi

Tunazingatia kuwa maudhui ya kitaifa kuwa muhimu katika mafanikio ya uendeshaji wa shughuli zetu. Hivyo tutahamasisha ushiriki wa kitaifa kwa;

- Kuimarisha utumiaji wa nguvu kazi na wakandarasi wa Uganda na Tanzania kupitia program za mafunzo na kusaidia makampuni ya ndani.
  - Kuimarisha ujuzi na uwezo kwa wenyeji.
  - kuanzisha ajira zilizo / na zisizo za moja kwa moja
  - kuunga mkono maudhui na manunuzi ya ndani
- Kuchangia maendeleo ya watu na kushiriki katika programu za maendeleo (usalama barabarani, upatikanaji wa nishati, kujenga uwezo)
- Kuimarisha miundombinu.

## Utoaji wa Ajira

Bomba litatoa ajira za muda mfupi (miaka 2-3) kwa wataalamu wenye ujuzi wa juu, ujuzi wa kati na vibarua. Inatarajiwa kwamba vibarua ambao watashiriki katika awamu ya ujenzi wa mradi pendekezwa watapatikana ndani ya nchi kutoka katika kila wilaya na hii itasaidia zaidi kukuza uwezo wa ndani.

**Watu 10,000 wataajiri wakati wa awamu ya ujenzi.**

# Kujidhatiti katika Ushirikishaji Wadau

Mradi wa EACOP unajidhatiti kushirikisha wadau wote wa muhimu kwa kufuata kanuni za ushirikishwaji, kuheshimu haki za binadamu, bila ya ubaguzi, uwezeshaji, uwazi na uwajibikaji. Ushirikishaji wa wadau utafanyika ili:

- Kuanzisha mahusiano mazuri ya kudumu na wadau.
- Utoaji wa taarifa kuhusu mradi kuwawezesha wadau kushiriki kikamilifu katika mchakato wote.
- Kufanya kazi kwa kushirikiana na wadau kuelewa dukuduku zao na kuzitafutia ufumbuzi.
- Kujidhatiti katika kushughulikia dukuduku za wadau kwakuzingatia haki na ufanisi.
- Kushughulikia mashauriano kwa uwazi stahiki kwa makundi tofauti ya wadau.

**EACOP PROJECT IN UGANDA**
TEAM - Total East Africa Midstream, Course View Towers,
Plot 21, Yusuf Lule Road,
P.O.Box 34867, Kampala – Uganda
Tel: 0800 216 000 (Toll free) or +256 (0) 204 916 000
Email: EACOP.info@total.com
www.eacop.com

**EACOP PROJECT IN TANZANIA**
TEAM – Total East Africa Midstream, 369 Toure Drive,
Ground Floor, Kilwa House, Oysterbay
P.O. Box 23917 Kinondoni Dar-es-Salaam, Tanzania.
Tel: 0800 780 068 (Toll free) or +255(0) 222 296 742
Email: EACOP.info@total.com
www.eacop.com

©April 2017. Haki zote zimehifadhiwa.
Hairuhusiwi kunakiri, kubadili au kuzalisha sehemu baadhi au yote ya chapisho hili bila taarifa kutoka kwa utawala wa Bomba la Mafuta Ghafi Africa Mashariki.

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

KUEND

RASILIMALI ASILIA YA MAFU

FURSA YA RASILIMALI ASILIA YA /